



Australian Government Disaster Recovery Payment

Australian Government Disaster Recovery Payment (AGDRP) ni malipo moja tu ili kukusaidia kama umeathirika kwa kiasi kikubwa na maafa yaliyotangazwa. Haya sio kwa uharibifu au usumbufu mdogo.

Kiasi unachoweza kukipata

Ikiwa unayastahili utapata:

- \$1,000 kwa mtu mzima
- \$400 kwa kila mtoto wa umri chini ya miaka 16.

Nani anaweza kuyapata

Ili kupata AGDRP unapaswa:

- kuwa mkaazi wa Australia au kushikilia viza inayostahili
- kuwa na umri wa miaka 16 au zaidi kwa wakati wa maafa au kupata malipo ya hifadhi ya kijamii
- kuridhi mahitaji ya ustahili wa Eneo la Serikali la Mtaa (LGA).

Lazima umeathirika vibaya na maafa yaliyotangazwa. Kwa mfano:

- ulijeruhiwa vibaya sana
- wewe ni jamaa wa karibu wa mraia au mkaazi wa Australia aliyefariki au ambaye amepotezwa
- maafa yaliharibu eneo lako kuu la makazi au linapaswa kuharibika
- kulikwa uharibifu mkubwa kwa mambo ya ndani ya eneo lako kuu la makazi
- maafa yale yamefunua mambo ya ndani ya eneo lako kuu la makazi kwa hali ya hewa
- eneo lako kuu la makazi limetangazwa kutokuwa sawa kimuundo
- maji machafu yamechafua mambo ya ndani ya makazi yako
- maafa yameharibu kabisa au kuharibu mali kuu ambayo unamiliki katika eneo lako kuu la makazi
- wewe ni mlezi mkuu wa mtoto anayekutegemea ambaye amepita yoyote ya hapo juu.

Ufafanuzi

- Eneo lako kuu la makazi ni mahali kuu ambapo una haki au leseni ya kuishi kwa kawaida. Haijumishi nyumba za likizo au mali ya uwekezaji.
- Mali kubwa ni mali ambayo ina thamani ya jumla ya \$20,000 au zaidi. Kwa mfano, hii inajumisha majengo, magari, misafara, matangi ya maji au mitambo mikubwa.
- Wewe ni mlezi mkuu wa mtoto kama mtoto huyo ni mtegemezi wako na hajafika umri wa miaka 16. Mlezi mkuu lazima awe na jukumu la kisheria kwa huduma ya kila siku, ustawi na ukuaji wa mtoto.

Jinsi ya kudai

Njia ya haraka sana ya kudai ni kwa mtandaoni. Utahitaji kuanzisha akaunti ya myGov na kuiunganisha na Centrelink ikiwa huna akaunti bado. Nenda kwa servicesaustralia.gov.au/mygovguides

Ikiwa unahitaji msaada wa kudai, unaweza kupiga simu kwa **180 22 66**. Simu hiyo ni wazi Jumatatu hadi Ijumaa, kutoka saa 2 asubuhi hadi saa 11 jioni (8 am hadi 5 pm) wakati wa mtaa. Unaweza kuomba mkalimani na tutakupangia mmoja kwa bure.

Ikiwa wewe ni mmoja wa wanandoa, nyote wawili mnaweza kuomba malipo haya. Wewe na mpenzi wako mnapaswa kufanya madai tofauti.

Nenda kwa servicesaustralia.gov.au/disaster kupata habari zaidi. Hii ni pamoja na:

- chaguzi za kudai
- LGAs zinazostahili
- jinsi ya kupata huduma zetu.

Kwa habari zaidi

- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/disaster kupata habari zaidi katika Kiingereza
- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/yourlanguage ambapo unaweza kusoma, kusikiliza au kutazama habari katika lugha yako
- piga simu kwa **131 202** kuongea nasi katika lugha yako kuhusu malipo na huduma ya Centrelink
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofautiana na watoaji huduma ya simu. Simu kwa nambari za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani ni bila malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda wao na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.

Kanusho

Habari iliyomo katika chapisho hili linakusudiwa tu kuwa mwongozo kwa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua ukitaka kuomba kwa malipo na kufanya ombi kuhusiana na hali yako maalum.



Australian Government Disaster Recovery Payment

The Australian Government Disaster Recovery Payment (AGDRP) is a one-off payment to help you if you are significantly affected by a declared disaster. It is not for minor damage or inconvenience.

How much you can get

If you are eligible you will get:

- \$1,000 per adult
- \$400 for each child younger than 16.

Who can get it

To get AGDRP you must:

- be an Australian resident or hold an eligible visa
- be 16 years or older at the time of the disaster or getting a social security payment
- meet Local Government Area (LGA) eligibility requirements.

You must have been adversely affected by a declared disaster. For example:

- you were seriously injured
- you are the immediate family member of an Australian citizen or resident who died or is missing
- the disaster destroyed your principal place of residence or it must be demolished
- there has been major damage to the interior of your principal place of residence
- the disaster has exposed the interior of your principal place of residence to the elements
- your principal place of residence has been declared structurally unsound
- sewage has contaminated the interior of your residence
- the disaster has destroyed or damaged a major asset or assets you own at your principal place of residence
- you are the principal carer of a dependent child who has experienced any of the above.

Definitions

- Your principal place of residence is the main place where you have a right or license to normally live. It doesn't include holiday homes or investment properties.
- A major asset is an asset or assets with a combined market value of \$20,000 or more. For example, this includes buildings, vehicles, caravans, water tanks or large scale machinery.
- You are a principal carer of a child if the child is your dependent and has not turned 16. The principal carer must have legal responsibility for the day-to-day care, welfare and development of the child.

How to claim

The fastest way to claim is online. You will need to set up a myGov account and link to Centrelink if you do not have one yet. Go to servicessaustralia.gov.au/mygovguides

If you need help with claiming, you can call **180 22 66**. The phone line is open Monday to Friday, from 8 am to 5 pm local time. You can ask for an interpreter and we will arrange one for free.

If you are a member of a couple, you can both claim this payment. You and your partner must make separate claims.

Go to servicessaustralia.gov.au/disaster for more information. This includes:

- claiming options
- eligible LGAs
- how to access our services.

For more information

- go to servicessaustralia.gov.au/disaster for more information in English
- go to servicessaustralia.gov.au/yourlanguage where you can read, listen to or watch information in your language
- call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It is your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.